

Big Fish



RIGHA'S SAFINA'S FARMING AQUA COMPANY LIMITED

Righa's Safina's Farming Aqua Company Limited (Big Fish) ni kampuni binafsi na ya kizalendo iliyosajiliwa na BRELA kwa namba ya usajili 110272. Makao yake makuu yapo Dar es salaam na imekwisha anza ufunguaji wa matawi katika mikoa mbalimbali nchi nzima ili iweze kuwezesha upatikanaji wa huduma zake kwa wakulima kwa wingi.

DIRA YA KAMPUNI

Dira ya kampuni ni kuwa mwezeshaji mkubwa wa ufugaji wa samaki, ufu gaji wa nyuki na upandaji na utunzaji wa misitu na miti ya matunda.

MALENGO YA KAMPUNI

Kampuni ina malengo yafuatayo:

- Kuzalisha vifaranga vya samaki vyenye ubora wa juu (sato, kambare na samaki wa mapambo) na kutoa elimu juu ya shughuli za ufugaji wa samaki wa kisasa.
- Kuongeza uzalishaji wa ndani wa samaki nchini Tanzania na kuweza kuwasafirisha nchi za nje ifikapo mwaka 2022.
- Kuhimiza ufugaji wa samaki na nyuki katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania.
- Kuwezesha na kubadilisha ufugaji wa samaki kuwa wa kisasa kwa ku tumia teknolojia na maar ifa ya kisasa.
- Kuufanya ufugaji wa samaki kuwa wenye faida na biashara ya inayokopesheka.
- Kuufanya ufugaji wa samaki kuwa wa kisasa kwa kuanzisha njia za kisasa kama utumiaji wa vizimba.
- Kufungua vituo mbalimbali vya kufugia samaki katika maeneo mbalimbali ya nchi.

WASHIRIKA WA KAMPUNI KATIKA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA KILA SIKU

Wafuatao ni washirika wa kampuni katika uendeshaji wa shughuli zetu:

1. FOODTECHAFRICA – Muungano wa makampuni yanayoongoza katika uvuvi.
2. LARIVE INTERNATIONAL – Maendeleo ya Bishashara ya Uholanzi
3. HOLLAND AQUA – Uundaji na utoaji wa huduma za uvuvi -Uholanzi.
4. VIQON WATER SOLUTIONS – Uundaji na utoaji wa huduma za uvuvi-Uholanzi.
5. TIL-AQUA INTERNATIONAL – Wataalamu wa jenetikia na utotoleshaji wa Uholanzi
6. EMBASSY OF THE KINGDOM OF THE NETHERLANDS- Ubalozzi wa Falme ya Uholanzi
7. GENAP WATERPROOF SOLUTIONS – Watatuzi wa matizo ya maji wa Uholazi
8. AQUA FISH -Wataalamu wa ufugaji wa samaki- Virginia – Marekani
9. PURDUE UNIVERSITY- Wataalamu wa utafiti na samaki-Marekani
10. Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – Kwa vifaranga vya samaki vyenye ubora wa hali ya juu na vyaku la vya ukuzaji wa samaki vya bei nafuu.
11. MWEA AQUAFISH FARM – Jimbo la Kambimbi Kirinyaga nchini Kenya – Wataalamu na watoaji wa vifaranga bora zaidi vya sato na samaki.

HUDUMA ZITOLEWAZO NA KAMPUNI

- Kuanzisha mashamba na vituo vya mfano vya samaki nchini kote Tanzania.
- Uzalishaji wa vifaranga bora vya sato , kambare na samaki wa mapambo.
- Uuzaji wa vyakula vyenye ubora wa hali ya juu na bei nafuu.
- Kutoa mafunzo kwa wafugaji wa samaki na mfumo wa umwagiliaji kwa mbogamboga na matunda (Kilimo mseto)
- Ujenzi wa mabwawa ya samaki na vizimba
- Uendeshaji wa shughuli za mabwawa ya samaki
- Uuzaji wa vifaa vyote vya uvuvi kama vile vifaa vya mashamba ya visimba na nailoni zinazozuia mabwawa kuvuja
- Teknologia ya YY (vifaranga)-Chakula cha samaki chenye ubora wa hali ya juu
- Utoaji wa huduma.

BigFish



HATUA TULIYOFIKIA KWA SASA. (MAMBO TULIYOYAFANYA)

- Umalizaji wa utafiti juu ya uzalishaji wa vifaranga bora zaidi vya sato na kambare (Utotoaji wa sato).
- Umalizaji wa kutengeneza mfumo wa maji na hewa kwa ajili ya ufugaji samaki kwa kutumia mabwawa, vizimba na mfumo wa RAS.
- Utafiti na ushauri juu ya mabwawa ya kisasa yenye ubora wa hali ya juu kwa ajili ya ufugaji samaki.
- Utafiti juu ya vizimba vya kufugia samaki vyenye obora wa hali ya juu.
- Tumefungua kituo na mabwawa ya samaki kwa ajili ya uzalishaji wa samaki kisasa na maendeleo ya ukuaji wa vifaranga nchi kavu (sato na kambare) maeneo ya Kigamboni Dar es salaam.
- Tumefungua sehemu ya kutotolea samaki, maabara na kituo cha ufugaji wa samaki nchi kavu eneo la Kigamboni Dar es Salaam.
- Maendeleo ya uzalishaji na ufugaji wa samaki maeneo ya Kibaha na Kiwangwa (Mkoa wa Pwani), Korogwe mkoani Tanga na Kisiwani wilayani Same .

MIRADI INAYOTARAJIWA NA KAMPUNI

Katika siku za usoni, nia yetu ni kuanza ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki na kuanzisha vituo vya mabwawa ya samaki maeneo ya Kibaha mkoani Pwani na Kisiwani mkoani Kilimanjaro. Ni dhamira yetu kuanzisha vituo vya ufugaji samaki wa kisasa kwa kutumia vizimba vya wakulima wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria.

MAWASILIANO YETU

RIGHA'S SAFINA'S FARMING AQUA COMPANY LIMITED
SANDUKU LA POSTA 38117 DAR ES SALAAM, TANZANIA.

SIMU YA KIGANJANI: + 255 758455284

SIMU ZA OFISINI + 255 713326073

+ 255 789520883

TOVUTI: www.bigfishtz.com; Barua pepe: info@bigfishtz.com

BigFish

